# K.P.S.E.A
# TATHMINI YA SHULE YA MSINGI
# TATHMINI YA MWISHO WA MUHULA WA 2, 2026
# GREDI YA 5 -

## KISWAHILI KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA
## Muda: 20 KILA MWANAFUNZI

**TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

Jina: ______________________________ Shule: ______________________________

Nambari ya Tathmini: ______________________________ Tarehe: ______________________________

Nambari ya Shule: ______________________________ Sahihi: ______________________________

**MAELEKEZO KWA WANAFUNZI**

1. Andika jina lako, jina la shule yako na nambari yako ya mthani katika nafasi ulizoachiwa.
2. Andika tarehe,nambari ya shule yako kisa weka sahihi yako.
3. Soma kila swali kwa makini
4. Mtahiniwa ahakikishe kuwa kurasa zote kwenye kijitabu hiki zimepigwa chapa.
5. Soma kifungu ulichopewa

JEDWALI LA ALAMA

| SEHEMU | INSHA | LUGHA | KUSI/KUZU | ASILIMIA (%) | KUZ 1 | KUZ 2 | KUF 1 | KUF 2 | KUK 1 | KUK 2 | CHI 1 | CHI12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| KIWANGO CHA ALAMA | ALAMA 20 | ALAMA 30 | ALAMA 30 | | 90-100 | 75-89 | 58-74 | 41-57 | 31-40 | 21-30 | 11-20 | 1-10 |
| POINTI | | | | | 8 POINTI | 7 POINTI | 6 POINTI | 5 POINTI | 4 POINTI | 3 POINTI | 2 POINTI | 1 POINTI |
| JUMLA YA ALAMA ZA MWANAFUNZI | | | | | | | | | | | | |

**Mwalimu asome kifungu kifuatacho kisha amwulize mwanafunzi maswali kwa sauti.**

Kandanda hupendwa na huchezwa kote duniani. Ni mchezo unaoleta watu pamoja kwa amani na furaha.

Zamani mchezo huu ulichezwa na wanaume pekee. Siki hizi, wanawake pia hucheza. Mchezo wa kandanada pia huitwa soka, ngozi ama kabumbu. Huchezwa na watu kumi na mmoja kila upande.

**Maswali**

1. Majina mengine yenye maana sawa na kandanda in ______________________
2. Mchezo wa soka huchezwa na watu wangapi kila upande? ______________________________
3. Kandanda hupendwa na kuchezwa wapi? _____________________________
4. Zamani mchezo huu ulichezwa na nani? __________________________

**SEHEMU YA PILI: KUSOMA KWA SAUTI (Alama 20)**

**Soma kifungu kifuatacho kwa sauti**

Wanyama wanaofugwa huitwa mifugo. Wanyama hawa ni kama mbuzi, kondoo, ng'ombe, ngamia na punda. Wanyama hawa wana faida nyingi sana. Mfugaji huwakamua ng'ombe ambao humpa maziwa ambayo humpa pesa nyingi akiyauza.

Maziwa pia hutumiwa kutengeneza siagi. Jbini hizi ni tamu sana. Kondoo hutupa sufi ambazo hutumiwa kutengeneza fulana. Maziwa ya mbuzi ni mazuri sana. Ngamia hutumiwa kubebea mizigo.

Maziwa yake pia hunywewa na watu wengine huamini kuwa ni dawa. Wanyama wote wanahitaji kutunzwa. Sharti waishi mahali safi na wapewe chakula cha kutosha ili wawe na afya nzuri.

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA**

**Mwongozo wa kusahisha**

**Sehemu ya Kwanza: Kusikiliza na Kuzungumza Majibu**

*(Mwalimu anasoma kifungu kwa sauti mara mbili, kisha anamwuliza mwanafunzi maswali haya ana kwa ana. Mwanafunzi anapaswa kujibu kwa sauti).*

1. Majina mengine yenye maana sawa na kandanda ni:

   **Soka, ngozi** au **kabumbu.** *(Mwanafunzi akitaja lolote kati ya haya anapewa alama).*

2. Mchezo wa soka huchezwa na watu wangapi kila upande?

   **Watu kumi na mmoja (11).**

3. Kandanda hupendwa na kuchezwa wapi?

   **Kote duniani.**

4. Zamani mchezo huu ulichezwa na nani?

   **Wanaume pekee.**

**Sehemu ya Pili: Kusoma kwa Sauti (Alama 20)**

**Mwongozo wa Mtahini / Mwalimu**

Wakati mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu **"Mifugo"**, mwalimu atumie vigezo vya tathmini vilivyopo hapa chini ili kurekodi alama zake. Mwalimu asimwongize mwanafunzi anapokwama isipokuwa tu akikaa kimya kwa zaidi ya sekunde tano.

**Rubriki ya Kutathmini Utamkaji na Ufasaha (Alama 20)**

| Kiwango cha Ustadi | Alama | Vigezo vya Kutathmini (Performance Indicators) |
|---|---|---|
| **Anazidi Matarajio** | **18 – 20** | * Anasoma kwa ufasaha wa hali ya juu bila kusita. |

| | | |
|---|---|---|
| | | * Anatamka maneno yote magumu kwa usahihi kabisa (mfano: *wanyama wanaofugwa, kutengeneza siagi, afya nzuri*).<br><br>* Anazingatia alama zote za uakifishaji (vituo na vitofautishi). |
| **Anatimiza Matarajio** | **12 – 17** | * Anasoma kwa mtiririko mzuri na kasi inayofaa.<br><br>* Anatamka maneno mengi kwa usahihi, akifanya makosa madogo yasiyozidi matatu.<br><br>* Anasita kidogo anapokutana na maneno marefu lakini anajisahihisha mwenyewe. |
| **Anakaribia Matarajio** | **07 – 11** | * Anasoma neno kwa neno (haunganishi sentensi kwa ufasaha).<br><br>* Anakosea kutamka msamiati wa kimsingi au anaruka baadhi ya maneno.<br><br>* Hazingatii alama za uakifishaji kama vile vituo kamili (.). |
| **Chini ya Matarajio** | **01 – 06** | * Anapata shida kubwa ya kutamka sauti na silabi za kawaida.<br><br>* Anasoma sentensi chache tu au anakataa kusoma kabisa.<br><br>* Anahitaji msaada wa mwalimu kwa kila neno. |